

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI IPOGOLO

S.L.P 1486, IRINGA.

KUMB. NA

MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

IRINGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPOGOLO

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Ipegolo mwaka, shule ya Ipegolo ipo umbali wa km 12 kusini mwa mkoa wa Iringa. Usafiri wa mabasi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha stendi kuu ya zamani. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe, mwanafunzi anatakiwa kuripotiti tarehe

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

1. Sare ya shule ni suruali mbili (upana inchi 8) kwa wavulana na sketi mbili urefu toka kwenye magoti sentimita thelathini (30)
2. Sare ya michezo kwa shule hii ni raba jozi moja na bukta moja rangi ya bluu kwa wavulana , raba jozi moja na bukta ya kijani na sketi yake kwa wasichana .
3. Kwa wanafunzi wa dini ya kiislamu , wasichana watavaa hijabu nyeupe , nusu kanzu nyeupe na sketi ndefu . (suruali haziruhusiwi)
4. Blauzi /mashati (2) nyeupe (tetron) mikono mifupi isiyoangaza
5. Viatu jozi mbili (2) nyeusi vyenye kamba visivyo na visigino virefu
6. Soksi nyeupe jozi mbili (2)
7. Sweta rangi ya bluu
8. Nywele fupi na nadhifu.

2.2 VIFAA VYA USAFI

1. Wavulana waje na jembe moja lenye mpini
2. Wasichana waje na ndoo mbili (02) za lita kumi (10)

2.3 VIFAA VYA KUJIFUNZIA

1. Daftari kubwa (counter book quire three) 10 , na daftari 10 za msomi kwa ajili ya mazoezi
2. Mkebe (mathematical set) 1
3. Peni , penseli na rula sm 30
4. Graph pad (kwa ajili ya michoro ya graph)
5. Aje na RIMU moja kwa ajili ya majaribio
6. Faili moja la plastiki (plastic file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake
7. Picha nne za (passport)

NB; mwanafunzi haruhusiwi kujipamba mapambo ya aina yeyote wala kufuga kucha.

3;0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

3.1 shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi , wazazi , wanafunzi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima .
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
3. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
5. Usafi wa mwili na mazingira ni muhimu sana.
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati , ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji sigara
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana na kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali za shule
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuo au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba
11. Kutoa mimba
12. Kugoma , kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu shuleni

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU

1. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospital ya serikali . Fomu hiyo itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi /mkataba wa kutoshiriki katika migomo , fujo na makosa ya jinai
3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0 TAFADHALI SOMA KWA UMAKINI MAELEZO / MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

KARIBU SANA IPOGOLO SEKONDARI

.....
KASSANGA , V.

MKUU WA SHULE

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
IPOGOLO SECONDARY SCHOOL**

P.O.BOX 1486, IRINGA – TANZANIA

To be completed by medical officer in respect of all form one entrant

Full name

Ageyear.....sex.....

Blood count (Red and White).....

Stool examination

Urine Analysis.....

Syphilis Test.....

Eye Test.....

T.B.Test.....

Ears.....

Chest

Spleen.....

Abdomen

ADDITIONAL INFORMATION

Eg. Physical or chronically of family disease etc.

.....
.....
.....

I certify that the above named student is fit to pursue studies

Signature

Designation.....

Section

Date

STUDENTS

You must bring this complete form , when you come to school . No student may be enrolled without certificate of physical fitness.

